2225 – 2414M

Diploma Programme
Programme du diplôme
Programa del Diploma

# Markscheme
# Barème de notation
# Esquema de calificación

## May / Mai / Mayo de 2025

## Kiswahili / Kiswahili / Kisuajili B

## Higher level – Paper 2 – Listening comprehension
## Niveau supérieur – Épreuve 2 – Compréhension orale
## Nivel Superior – Prueba 2 – Comprensión auditiva

12 pages/páginas

International Baccalaureate
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

© International Baccalaureate Organization 2025

All rights reserved. No part of this product may be reproduced in any form or by any electronic or mechanical means, including information storage and retrieval systems, without the prior written permission from the IB. Additionally, the license tied with this product prohibits use of any selected files or extracts from this product. Use by third parties, including but not limited to publishers, private teachers, tutoring or study services, preparatory schools, vendors operating curriculum mapping services or teacher resource digital platforms and app developers, whether fee-covered or not, is prohibited and is a criminal offense.

More information on how to request written permission in the form of a license can be obtained from https://ibo.org/become-an-ib-school/ib-publishing/licensing/applying-for-a-license/.

© Organisation du Baccalauréat International 2025

Tous droits réservés. Aucune partie de ce produit ne peut être reproduite sous quelque forme ni par quelque moyen que ce soit, électronique ou mécanique, y compris des systèmes de stockage et de récupération d’informations, sans l’autorisation écrite préalable de l’IB. De plus, la licence associée à ce produit interdit toute utilisation de tout fichier ou extrait sélectionné dans ce produit. L’utilisation par des tiers, y compris, sans toutefois s’y limiter, des éditeurs, des professeurs particuliers, des services de tutorat ou d’aide aux études, des établissements de préparation à l’enseignement supérieur, des fournisseurs de services de planification des programmes d’études, des gestionnaires de plateformes pédagogiques en ligne, et des développeurs d’applications, moyennant paiement ou non, est interdite et constitue une infraction pénale.

Pour plus d’informations sur la procédure à suivre pour obtenir une autorisation écrite sous la forme d’une licence, rendez-vous à l’adresse https://ibo.org/become-an-ib-school/ib-publishing/licensing/applying-for-a-license/.

© Organización del Bachillerato Internacional, 2025

Todos los derechos reservados. No se podrá reproducir ninguna parte de este producto de ninguna forma ni por ningún medio electrónico o mecánico, incluidos los sistemas de almacenamiento y recuperación de información, sin la previa autorización por escrito del IB. Además, la licencia vinculada a este producto prohíbe el uso de todo archivo o fragmento seleccionado de este producto. El uso por parte de terceros —lo que incluye, a título enunciativo, editoriales, profesores particulares, servicios de apoyo académico o ayuda para el estudio, colegios preparatorios, desarrolladores de aplicaciones y entidades que presten servicios de planificación curricular u ofrezcan recursos para docentes mediante plataformas digitales—, ya sea incluido en tasas o no, está prohibido y constituye un delito.

En este enlace encontrará más información sobre cómo solicitar una autorización por escrito en forma de licencia: https://ibo.org/become-an-ib-school/ib-publishing/licensing/applying-for-a-license/.

1. For questions where candidates must write their answers, do not award the mark if the answer is incomplete, or if there is additional information that is irrelevant or shifts the focus of the answer. However, accept other words with the same meaning as the correct answers in the markscheme.
2. Accept spelling and grammatical mistakes provided they do not change the meaning of the answer.
3. For questions where candidates choose an answer from options, if two answers are given – one in the box and one outside – only mark the answer inside the box.
4. Words inside brackets in this markscheme are optional: candidates may include these words in their answer, but they are not essential for the mark to be awarded. If there is more than one possible answer to a question, these answers are indicated by a slash (/).
5. This markscheme must be read in conjunction with the Marking Instructions for the relevant component on IBIS.

1. En ce qui concerne les questions pour lesquelles les candidats doivent rédiger leurs réponses, n’attribuez pas le point si la réponse est incomplète, ou s’il y a des informations supplémentaires qui ne sont pas pertinentes ou qui modifient l’objet de la réponse attendue. Néanmoins, l’utilisation de mots ayant le même sens que les bonnes réponses est acceptée dans le barème de notation.
2. Les erreurs d’orthographe et de grammaire sont acceptées si elles ne changent pas le sens de la réponse.
3. En ce qui concerne les questions pour lesquelles les candidats doivent choisir une réponse parmi plusieurs propositions, s’ils ont donné deux réponses différentes, l’une à l’intérieur de la case et l’autre en-dehors, ne prenez en compte que la réponse qui se situe dans la case.
4. Les mots entre parenthèses dans ce barème de notation sont facultatifs : les candidats peuvent les inclure dans leur réponse, mais ils ne sont pas essentiels pour justifier l’attribution du point. S’il y a plus d’une réponse possible à une question, celles-ci sont indiquées par une barre oblique (/).
5. Ce barème de notation est à lire parallèlement aux instructions de notation disponibles sur IBIS pour la composante concernée.

1. En las preguntas en las que los alumnos deban responder por escrito, no otorgue la puntuación si la respuesta está incompleta, o si aportan detalles adicionales que cambian el enfoque o no son pertinentes. No obstante, acepte otras palabras con el mismo significado que las respuestas correctas en el esquema de calificación.
2. Acepte los errores de ortografía y gramática, siempre y cuando no modifiquen el significado de la respuesta.
3. En las preguntas en las que los alumnos deban elegir una opción, si se han escrito dos respuestas (una dentro de la casilla y la otra fuera), puntúe únicamente la que esté dentro de la casilla.
4. Las palabras entre corchetes en este esquema de calificación son opcionales: los alumnos pueden incluirlas en la respuesta, pero no son fundamentales para que se otorgue la puntuación. Si hay más de una respuesta posible a una pregunta, esto se indica con una barra (/).
5. Este esquema de calificación debe leerse junto con las instrucciones para la corrección del componente en cuestión disponibles en IBIS.

**Kifungu A**

| Swali | | Jibu lengwa | Kubali | Usikubali | Alama |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | | zawadi ya siku ya kuzaliwa | Kwa siku ya kuzaliwa (Eva) | | **1** |
| 2. | | udhamini | | | **1** |
| 3. | | kutamka maneno ya nyimbo | | | **1** |
| 4. | | walipigiana makofi | walikumbatiana | | **1** |
| 5. | | chuo kikuu | | | **1** |
| | | | | **Jumla** | **5** |

**Kifungu B**

| Swali | | Jibu lengwa | Kubali | Usikubali | Alama |
|---|---|---|---|---|---|
| **6.** | | C, D, G, H, J | | | **5** |
| **7.** | | wote wawili | | | **1** |
| **8.** | | Mwanafunzi | | | **1** |
| **9.** | | wote wawili | | | **1** |
| **10.** | | Mhifadhi | | | **1** |
| **11.** | | wote wawili | | | **1** |
| | | | | **Jumla** | **10** |

**Kifungu C**

| Swali | | Jibu lengwa | Kubali | Usikubali | Alama |
|---|---|---|---|---|---|
| **12.** | | kutoweka (kwa lugha / katika miongo michache) | | | **1** |
| **13.** | | kuzihifadhi | | | **1** |
| **14.** | | 21 Februari | Mwezi wa Pili, tarehe 21 | | **1** |
| **15.** | | utambulisho (wa jamii) | | | **1** |
| **16.** | | kulinda uanuwai wa lugha | | | **1** |
| **17.** | | B | | | **1** |
| **18.** | | C | | | **1** |
| **19.** | | B | | | **1** |
| **20.** | | A | | | **1** |
| **21.** | | C | | | **1** |
| | | | | **Jumla** | **10** |

**Kifungu A**

**Sasa utasikia mahojiano kati ya mshindi wa shindano la kuimba na mwandishi wa habari.**

| | |
|---|---|
| Mwandishi wa habari | Eva, asante kwa kujiunga nami leo kuzungumzia ushindi wako wa shindano la kuimba la Nyota Mpya. Hebu nikumbushe, mapenzi yako ya kuimba yalianza lini? |
| Eva | Nimependa kuimba tangu nilipokuwa mdogo. Rafiki zangu na mimi tulikutana jioni baada ya shule na tulifanya mazoezi ya kuimba. Mama yangu alitaka niende shule ya muziki ili kupata mafunzo lakini sikutaka kufanya hivyo kwani nilihisi ingekuwa taabu kwangu. Mwishowe, kwa zawadi ya siku yangu ya kuzaliwa, alinilipia madarasa kumi ya kuimba. |
| Mwandishi wa habari | Alaa kumbe! Ulifanya nini baada ya hayo madarasa? |
| Eva | Niliyafurahia sana na kuamua kujisajili kwa muda mrefu zaidi. Nilifurahia kuona uwepo wa madarasa ya kila aina. Tatizo pekee lilikuwa uwezo wangu duni wa kipesa. Sikuweza kumudu masomo ingawa yalikuwapo mengi yaliyofundishwa. Kwa bahati nzuri, niliona tangazo la udhamini wa madarasa ya kuimba kwa wote. Ingawa mimi si mshindani, nilitaka kufanikiwa kwa kudhaminiwa. |
| Mwandishi wa habari | Ulipaswa kufanya nini ili kupata udhamini huo? |
| Eva | Ilibidi kufanya mazoezi kwa ajili ya mtihani wa kuimba na nikashinda nafasi. Kwa kweli ni masomo hayo yaliyonisaidia kushinda shindano la Nyota Mpya na kupata uzoefu ambapo nilikutana na watu wengine waliopenda kuimba. |
| Mwandishi wa habari | Tafadhali Eva, Tuambie zaidi kuhusu shindano. Je, ulipata changamoto gani hasa? |
| Eva | Ilinibidi kujifunza aina nyingi za nyimbo ambazo zilikuwa ngumu. Nililazimika kujifunza nyimbo ya kitamaduni ya Wakikuyu; kwa vile sizungumzi lugha yao, ilibidi kutafuta msaada wa mwenyeji anisaidie kutamka maneno ya nyimbo. Pia, nilihangaika kuimba Taarab ya Kiswahili licha ya kufanya mazoezi mengi. Ninashukuru nilifanikiwa. |
| Mwandishi wa habari | Tuambie kuhusu washiriki wengine. Je, walikuwaje? |
| Eva | Nilihisi kila mtu alikuwa na ushindani mkubwa, jambo ambalo lilinifanya niwe na wasiwasi sana lakini pia waliungana mkono kwa kupigiana makofi na kukumbatiana. |
| Mwandishi wa habari | Vizuri. Kwa hivyo ungewahimiza wengine kushiriki katika shindano hilo? |

| | |
|---|---|
| Eva | Bila shaka ni uzoefu mzuri kwangu. Lakini, hata hivyo kwa miezi kabla ya mashindano, mtu huwa na wasiwasi na inabidi kufanya kazi kwa bidii. Nilikuwa na wasiwasi kwamba ingeathiri kazi yangu ya shule. Nilikuwa na bahati kwamba familia yangu na marafiki waliniunga mkono kwa kiasi kikubwa. |
| Mwandishi wa habari | Kwa hivyo, una mipango gani kwa miaka ijayo? |
| Eva | Nimegundua kwamba kuna vijana wengi wanaopenda kuimba na wanaotamani fursa za kitaaluma. Tumaini langu ni kuwa, hatimaye, niwe na kampuni kubwa. Familia yangu inataka niende chuo kikuu kwanza. Ingawa sitaki kufanya hivyo, itabidi nitume maombi. |
| Mwandishi wa habari | Asante, Eva, nakutakia kila la kheri. |

**Kifungu B**

**Utasikia mazungumzo kati ya mhifadhi wa mbuga na mwanafunzi, siku moja kabla ya safari ya kwenda Hifadhi ya Kitaifa ya Serengeti.**

| | |
|---|---|
| Mhifadhi | Vipi mambo! Uko tayari kwa safari ya kesho? |
| Mwanafunzi | Bila shaka! Mimi nina hamu sana ingawa si wote tunaohisi hivyo. Safari yetu ya ndege kutoka London ilichukua saa 13 na kwa bahati mbaya mmoja kati ya wanafunzi watatu waliokuwa wakisafiri kwa ndege kwa mara ya kwanza, alipoteza begi lake. |
| Mhifadhi | Masikini, je alibeba mzigo mdogo wa mkononi? |
| Mwanafunzi | Ndiyo. Lakini pia, shule yetu imeshiriki katika mchakato huu wa kutembeleana kimasomo kwa miaka 25 sasa. Walimu wetu wawili wamekuwa wakija katika kempu hii hapa kwa miaka mingi sasa na wamekuwa wakiacha baadhi ya mashati na suruali kwenye sanduku dogo. |
| Mhifadhi | Jambo zuri kwa dharura kama hii. Je, una hamu ya kufanya nini kwenye safari hii? |
| Mwanafunzi | Kuwaona wanyama katika makazi yao ya asili. Nina hamu ya kuwaona fisi. Filamu huwaonyesha kuwa waovu na wenye fujo. Katika filamu moja, wao ni washirika wa mjomba mwovu wa mfalme simba ambaye anataka kuangamiza maisha ya wanyama wote nchini kwao. Je, ndivyo walivyo fisi? |
| Mhifadhi | Sidhani, ingawa fisi hula mizoga, wao ni wawindaji wazuri kwa sababu wana taya zenye nguvu. Pia wana akili sana. Koo za fisi ni za mfumo wa kike ambapo watawala ni fisi jike. Muundo wao wa utawala hufuata majike, watoto wa kike hurithi utawala kutoka kwa akina mama fisi. |
| Mwanafunzi | Kumbe! Kwa kawaida nisingetaka kununua zawadi yoyote inayohusiana na fisi lakini nimeamua kufanya hivyo sasa. Siwezi kununua zawadi katika hoteli lakini nitaenda sokoni ambapo ninaweza kununua zawadi kwa familia yangu. Zitakuwa bei nafuu huko na kila mtu atapenda zawadi zake. |
| *** | |
| Mhifadhi | Tutakapokuwa safarini kutoka mbugani, tutapitia katika kijiji kimoja na utaweza kununua zawadi unazotaka. |
| Mwanafunzi | Itakuwa vizuri. Ninathamini kulindwa kwa mazingira hivyo ninataka zawadi rafiki kwa mazingira. Tumekuja katika safari hii ili kuelewa wanyama pori kwenye mazingira asilia. |
| Mhifadhi | Kulinda mazingira ni muhimu. Shule yenu inafanya nini hasa kuhusu ulinzi wa mazingira? |

| | |
|---|---|
| Mwanafunzi | Tunakutana mara moja kwa wiki kwa mradi wetu unaohusika na kulisha ndege pori. Tunaning'iniza vyakula vya ndege kuzunguka shule. Pia tuna uwanja wa maua mwitu ambao tumeupanda wenyewe. Tuliwapa wanafunzi wenzetu changamoto ya kupanda maua na sasa tuna nyuki wanaotengeneza asali nyingi. |
| Mhifadhi | Vizuri sana. Hata sisi tunatumia asali ya kienyeji inayotoka hapa hapa kwetu. Una bahati ya kuweza kujishughulisha na mazingira ya asili kwa njia zenye maana. Sisi kama walinzi wa mbuga, jukumu letu kuu ni kulinda na kuhifadhi maeneo ya mbuga. |
| Mwanafunzi | Hebu niambie wajibu wako hasa ni upi? |
| Mhifadhi | Baadhi ya mambo muhimu tunayofanya ni pamoja na kusimamia sheria za kupambana na ujangili na hivyo kupunguza mahitaji ya bidhaa zinazotengenezwa kutokana na wanyama pori kama fisi. Tunafanya kazi kwa bidii ili kulinda makazi ya wanyama pori. |
| Mwanafunzi | Ujangili ni tatizo kubwa linalokera. Si hakikabisa. Ndio tunajitahidi kupingana nalo. |

**Kifungu C**

**Utasikia mazungumzo kuhusu maadhimisho ya Siku za Lugha**

| | |
|---|---|
| Chege | Jina langu ni Chege na mimi ni mwana isimu. Nina shauku kubwa ya kuzungumza kuhusu lugha na uhusiano uliopo na tamaduni pamoja na jamii tofauti. |
| | Kuna zaidi ya lugha 7,000 zinazozungumzwa duniani kote, ingawa zipo lugha nyingine zinazotumiwa zaidi, kama vile Kiingereza, Kifaransa na Kireno. Kuna uwezekano mkubwa wa kutokea shida kama lugha nyingi za kiasili kutoweka katika miongo michache ijayo. Baadhi ya hizo zinazungumzwa na jamii ndogo hivi leo na si zote zenye maandishi. Kuandikwa kwa lugha ni muhimu ili kuzihifadhi. Kwa hivyo sote tujitahidi kuandika lugha zetu. Katika mazungumzo yangu leo ningependa kuwafahamisha watu kuhusu umuhimu wa lugha na jinsi jamii tofauti duniani zinavyosheherekea lugha zao. |
| | Tarehe 21 Februari ni Siku ya Kimataifa ya Lugha Mama na huadhimishwa kila mwaka. Ni siku ambayo lugha nyingi na tofauti za kitamaduni katika nchi mbalimbali huadhimishwa. Ni muhimu kwa sababu, ingawa baadhi ya lugha zina umaarufu duniani kote, lugha za kienyeji huathiri utambulisho wa jamii. Lugha zote huathiri namna yetu ya kufikiri, hujenga mwonekano wetu wa ulimwengu na hufufua urithi wa lugha wa jamii tofauti. Wanadamu huwasilisha hisia na mawazo kupitia lugha. Kutokana na kasi ya ulimwengu wetu na jinsi unavyobadilika haraka, watu kote ulimwenguni huadhimisha Siku ya Kimataifa ya Lugha ya Mama ili kulinda uanuwai wa lugha. Maadhimisho ya lugha ya Mama hufanywa kimataifa tofauti na siku ya Lugha ya Kiswahili Duniani ambayo huadhimishwa na mataifa machache. |
| *** | |
| Chege | Kwa Kiswahili, mambo yalianza katika miaka ya 1950 wakati Radio ya Umoja wa Mataifa ilipoanzisha kitengo cha lugha ya Kiswahili ambapo vipindi vya matangazo vilianza kutangazwa kwa Kiswahili. Kwa kawaida lugha zilizotumiwa zilikuwa Kiingereza na Kifaransa. Pia, hivi karibuni Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) limechukua hatua ya kusonga mbele zaidi na kuchagua tarehe 7 Julai kuwa Siku ya Lugha ya Kiswahili Duniani. Kiswahili ni lugha ya kwanza ya Kiafrika kupata heshima ya kuwa na siku ya kukiadhimisha. |
| | Kwa kawaida siku ya Kiswahili huadhimishwa kwa shughuli mbalimbali, ikiwa ni pamoja na maonyesho ya lugha, vipindi vya kusimulia hadithi, na maonyesho ya kitamaduni. Sherehe hiyo hutayarishwa na kuandaliwa na watu wanaojitolea kutokana na kiingilio kwenye maonyesho kuwa bure kwa wote. Mwishoni wote hurusha fataki. |
| | Kuchaguliwa na kuadhimishwa kwa tarehe 7 Julai kuna muktadha wa kihistoria unaoshirikisha nchi ya Tanzania. Siku kama hiyo, mwaka 1954, chama cha siasa, Tanganyika African National Union (TANU) kilizaliwa chini ya rais wa kwanza wa Tanzania, hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Sababu kuu kwa Nyerere kuchagua Kiswahili kama lugha ya taifa ni jinsi inavyounganisha watu. Pia Kiswahili kilitumiwa kama lugha ya kupigania uhuru na kuondokana na ukoloni. |

| | |
|---|---|
| | Hivi sasa tarehe 7 Julai ni likizo ya umma Tanzania ambapo watu husheherekea siku ya Saba Saba. Saba Saba huwa na Maonyesho ya Biashara. Nchini Kenya, tarehe hiyo inaadhimisha siku ya Haki za Binadamu. |
| | Asanteni kwa kunisikiliza na ninategemea nyote mtaadhimisha lugha zenu. |